

UNAPOANDAA VYAKULA KUMBUKA

- Tumia malighafi zilizoko katika mazingira yako.
- Tengeneza chakula chenye ubora unaokidhi mahitaji.
- Malighafi zihifadhiwe vizuri sehemu kavu zikiwa zimekauka kwani zinaweza kusababisha magonjwa kwa kuku.
- Hata kama malighafi ni kavu zikaguliwe kuhakikisha hazina ukungu.



Mashudu ya karanga



Mtama



Unga wa Mifupa

OFISI YA MKUU WA MKOA RUVUMA,
Simu Na: 2602256/2602238 Fax
Na: 2602144 Anwani ya Posta:
S.L.P. 74, Songea
Email:

ras.ruvuma.@tamisemi..go.tz
aeps@ruvuma.go.tz
Kwa mawasiliano zaidi wasiliana na
Afisa Ugani aliyeko karibu na wewe.

AU

Wataalam Ofisi Ya Mifugo Mkoa
kwa Simu Na. +255765689488,
+255752521869, +255753431915



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKAL ZA MITAA



**UTENGENEZAJI WA VYAKULA
VYA KUKU**



Mashudu

MKOA WA RUVUMA

MWONGOZO WA UTENGENEZAJI WA VYAKULA VYA KUKU

UTANGULIZI

UTENGENEZAJI WA VYAKULA VYA KUKU

Wafugaji wengi wanapata faida ndogo kutokana na gharama kubwa ya chakula cha kuku au wengine kutokuwa na uelewa wa namna ya kuandaa chakula hicho. Vyakula vya kuku vinaweza kupatikana madukani au kwa kutengenezwa na mfugaji mwenyewe. Ili kuku aweze kukua haraka na kuzalisha mazao mengi na bora ni lazima chakula kitengenezwe katika mchanganyiko wenye uwiano mzuri uliopendekezwa.

KABLA YA KUTENGENEZA CHAKULA CHA KUKU LAZIMA MFUGAJI AFAHAMU MAMBO HAYA

- Upatikanaji wa vyakula vya aina mbalimbali
- Viini lische vinavyohitajika na umri na aina tofauti ya kuku mfano vifaranga wanahitaji protini asilimia 18 hadi 22. kuku wa mayai kalishamu 3-4%.
- Viwango vya uchanganyaji wa chakula kulingana na umri.
- Kiasi cha viini lische kama protini, wanga, madini, vitamin nk.
- Aina ya kuku mfano vifaranga, kuku wakubwa, majogoo, kuku wa mayai, kuku wa nyama.

Kuna njia mbalimbali za kutengeneza chakula cha kuku lakini katika makala hii tutajifunza njia moja ya kuangalia viwango vinavyohitajika (inclusion level) kwa mchanganyiko wa kilo 100.

- Vyakula vya protini ya mimea visizidi 25kg mfano soya, pamba, alizeti n.k.

- Vyakula vya wanga unaweza weka 15-55kg mfano mahindi, mtama, ulezi, mchele n.k
- Viambata vingine (additives) mfano lysine, methionine visizidi 2kg
- Madini mengine kama Ca, P, Zn nk visizidi 5kg
- Chumvi isizidi asilimia 1kg
- Vitamin unawza tumia ya maji

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KATIKA UCHANGANYAJI WA CHAKULA CHA KUKU

- Vyakula vya protini ya wanyama kama damu inas-hauriwa isizidi asilimia 5% kwasababu mmeng'enyoyake wake ni mdogo.
- Baadhi ya vyakula kama soya isipo kaangwa au kuchemshwa vizuri inakuwa na viambata sumu (trypsin inhibitor) hii huweza kusababisha vifo kwa kuku.
- Unapochanganya vyakula ni muhimu kuwepo kwa aina zaidi ya moja ya chakula cha protini ya wanyama na mimea na wanga.
- Vyakula visipohifadhiwa vizuri huweza kutengeneza sumu kuvu (mycotoxin) ambayo huweza kusababisha madhara kwa wanyama. Hivyo ni muhimu kuhifadhi vyakula vikiwa vimekauka

FAIDA ZA KUCHANGANYA VYAKULA VYA KUKU

- Inapunguza gharama za vyakula vya kuku inapunguza gharama kwa asilimia kubwa mfano mfuko wa kilo 50 dukani unapatikana kwa gharama ya shilingi 60,000/= unapochanganya unaweza gharama hizo ukazalisha kiasi cha kilogramu 100 za chakula hicho.
- Ukuaji wa kuku huongezeka kutokana na uhakika wa upatikanaji wa chakula.
- Uzalishaji huongezeka kutokana na uhakika wa

ANGALIZO:

Unaponunua malighafi za vyakula vya kuku mfano soya, alizeti, pamba, damu, chokaa, mifupa, premix, pamba za mahindi unapofika nyumbani andaa turubali kisha changanya mchanganyiko wako vizuri kwa kutumia beleshi hii ni njia rahisi kwa wafugaji wadogo wasio na mashine za kuchanganyia. Hakikisha mchanganyiko wako ni wa kilo mia (100kg) na una virutubisho vyote kulingana na mahitaji ya mifugo yako kama vile kuku, vifaranga, majogoo au mitetea kila umri na rika una resheni

Jedwali hapo chini ni Mfano wa Chakula cha vifaranga kuanzia wiki ya kwanza hadi nane (1-8) kwa mchanganyiko wa kilo mia (100kg)

Aina ya vyakula	Kiasi (Kilo)
Unga wa nafaka kama mahindi au mtama	40
Pamba za mtama, mahindi, uwele,	27
Mashudu ya, alizeti, ufuta karanga au pamba n.k	20
Unga wa mifupa au chokaa ya kuku	2.25
Dagaa au mabaki ya samaki	10
Chumvi ya jikoni	0.5
Virutubisho (Premix)	0.25
Jumla	100